**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 2, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya Sudana

*Antony Kago Waithiru*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Laikipia, S.L.P. 1100 – 20300. Nyahururu, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: kagoantony3@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*16 Desemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Taashira, Umitindo, Wahusika, Mbinu, Ukoloni mamboleo.*

**IKISIRI**

Makala haya yanahusu uhakiki wa taashira za wahusika katika tamthilia ya Sudana. Makala haya yalinuia kubaini wahusika wanaosawiriwa kitaashira na waandishi. Pia, yalinuia kujadili namna waandishi walivyowatumia wahusika kitaashira kuwasilisha ujumbe lengwa. Makala haya yaliyojikita katika nadharia ya umitindo yanadhihirisha kuwa taashira imetumika katika tamthilia husika kama mbinu fiche na kwepi ya kuikosoa na kuielekeza jamii. Baadhi ya masuala ambayo yameangazia ni pamoja na viongozi dhalimu, ubaguzi, ukabila, tamaa na ubinafsi. Kadhalika, yanaeleza kuwa taashira imetumika vyema katika tamthilia hii madhali imeauni waandishi kuepuka uwezekano wa kusawiri masuala yanayokumba jamii paruwanja, jambo ambalo lingenyima kazi yenyewe mnato. Badala yake, kazi yenyewe imeonyesha kuwa waandishi walifinyanga lugha na kuwasawiri wahusika wa kawaida kwa njia mpya na ya kutendesa kupitia taashira. Yanaonyesha tadi na inda zinazotumiwa na baadhi ya watawala katika mataifa yanayoinuka kiuchumi kujinufaisha kibinafsi pamoja na vikaragosi wao. Isitoshe, makala haya yamedhihirisha jinsi viongozi wa mataifa hayo hudhibitiwa na watawala katika mataifa yaliyoinuka kiuchumi na kusababisha ulofa wa wananchi katika mahusiano yanayofichika katika ukoloni mamboleo. Yaliongozwa na nguzo kuu za nadharia ya umitindo. Nadharia ya umitindo ina nguzo kadhaa muhimu lakini makala haya yaliongozwa na nguzo tatu kuu ambazo ni ile ya kiwango cha umbo, ya kiwango cha kisemantiki, pamoja na ile ya mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo baina ya wahusika.

**APA CITATION**

Waithiru, A. K. (2022). Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya Sudana. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 124-130. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010

**CHICAGO CITATION**

Waithiru, Antony Kago. 2022. "Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya Sudana". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 124-130. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010.

**HARVARD CITATION**

Waithiru, A. K. (2022) "Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya Sudana", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 124-130. doi: 10.37284/jammk.5.2.1010.

**IEEE CITATION**

A. K. Waithiru "Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya Sudana", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 124-130, Dec. 2022.

**MLA CITATION**

Waithiru, Antony Kago. "Tathmini ya Taashira za Wahusika Katika Tamthilia ya Sudana". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Dec. 2022, pp. 124-130, doi:10.37284/jammk.5.2.1010.

## UTANGULIZI

Waithiru, Nabea na Onyango (2021) wanaeleza kuwa mbinu ni vipengele vya kimtindo na kimuundo ambavyo hupatikana katika kazi yoyote ya kifasihi kama vile tamthilia. Mathalani, tamthilia ya *Sudana* (2006) ya Kimani Njogu na Alamin Mazrui imetumia mbinu ya taashira kupitia usawiri wake wa wahusika kuwasilisha ujumbe lengwa. Kulingana na Waithiru (2022a), taashira ni aina ya tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu hutumiwa kuwakilisha kitu kamili au kingine kinachohusiana nacho. Neno au jina kuchukua nafasi ya neno au jina lingine linalohusishwa nalo. Ni mbinu ambayo hutumiwa na baadhi ya waandishi kuashiria dhana zinazokanganya, hisia pamoja na hali za kiakili.

Katika tamthilia hii, Alamin Mazrui na Kimani Njogu wanaangaza utandawazi kupitia wahusika, vifaa na maumbile. Katika shairi tangulizi, watunzi wanaeleza jinsi Wazanji walipigania uhuru ambao hatimaye uligeuka ndoto. Meli ya Wazanji inayoabiri baharini inakumbwa na matatizo ya kiufundi na kuhatarisha maisha ya abiria. Ufuoni, wanaona Wamerope na kuomba msaada kutoka kwao. Wamerope wanawarushia kamba wanazofunga katika mashua na kuvutwa na Wamerope hadi ukingoni. Kumbe hisani ya Wamerope imegubikwa na unafiki. Punde, Wazanji wanaanza kufanyishwa kazi ngumu na Wamerope. Kadhalika, mashua yao inabomolewa na mbao zake kutumiwa kukarabati mashua ya Amerope iliyochakaa. Kitaashira bara la Afrika lanyonywa na mataifa ya Marekani na Uropa. Waandishi wanaashiria changamoto ambazo Waafrika hukumbana nazo katika harakati za kupigania uhuru na kulilinda bara la Afrika dhidi ya unajisi wa mataifa ya Uropa na Marekani (Waithiru, 2022b). Mateso wanayoshindiliwa Wazanji ni ya uchungu ikiwemo kuwekwa vifungoni, kuchapwa, kukatwa viungo vya miili na kubakwa. Hatimaye Wazanji wanapanga njama na kuanzisha vita vya ukombozi dhidi ya Wamerope ambapo damu nyingi inamwagika, ya wadhalimu kwa wadhulumiwa.

## DHANA YA TAASHIRA

Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 208), taashira ni aina ya tamathali ya usemi ambapo jina la sehemu ya kitu hutumiwa kuwakilisha kitu kamili au kingine kinachohusiana nacho. Dhana ya taashira ni muhimu sana katika uchanganuzi wa taashira za wahusika katika tamthilia ya *Sudana* (2006). Nauta (1972) alitoa maoni kuwa ishara huwakilisha kifikira hali ya kitu kinachoashiriwa na kwamba uhusiano wa ishara na kiwakilishwa ni wa kidhahania. Mawazo haya yanaelekeza kwamba uashiriaji ni mbinu ya kuviwasilisha vitu kwa kutumia ishara. Kwa upande mwingine, Madumula (2009) alisema kuwa neno ishara kama istilahi ya kifasihi, ni lile lililo sawa na kitenzi chenye maana ya 'tupia pamoja' na nomino yake huwa na maana ya 'alama', 'nembo' au 'dalili' au 'ishara'. Hamad (2017) alidokeza kuwa taashira ni mbinu ya mwandishi kutumia kitu chenye uhai au kisicho na uhai kukiwakilisha na kitu kingine chenye uhai au kisichokuwa na uhai. Kadhalika, Waithiru (2022b) na Mbuvi (2014) wakiangazia mbinu ya taashira wanaeleza kuwa taashira ni neno au fungu la maneno ambalo huwakilisha hali fulani. Maoni yao yalichangia makala haya katika kufafanua dhana ya taashira.

Msimamo wa makala haya ni kuwa taashira kama ishara hutumiwa kuwakilisha kitu kingine. Taashira

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010

huwakilisha kitu au hali halisi pasipo lazima ya kulandana. Huwa na asili katika tamaduni mbalimbali. Kuna taashira za kimataifa kama vile njiwa – taashira ya amani, mawingu – taashira ya mvua; taashira za trafiki – nyekundu kuashiria kukataza magari au watu kupita, na kijani kuashiria magari au watu wapite (Waithiru, 2022b). Madumula (2009) anatahadharisha kuwa, katika fasihi msanii anaweza kutumia vitu fulani kusimamia ishara zake mwenyewe na kwa makusudi yake binafsi na kwa kufanya hivyo, akawa amekiuka maana zilizozoeleka au za kiutamaduni. Wilson (1998) akiifasiri taashira, anasema kuwa ni ishara: yambwa (kitu), mtu, wazo, alama, nembo inayoonyesha kitu kingine. Wilson anaeleza kuwa, ishara huwa halisi kuliko uhalisi wenyewe na huwa na nguvu nyingi za kuathiri maisha ya binadamu. Katika maisha ya kila siku, watu huzingirwa na aina mbalimbali za taashira kama vile taashira za barabarani, taashira zinazosikika, taashira za hisabati, taashira za maneno na taashira za hadhi ambazo hufasiriwa na watu na hivyo kuibua maana mbalimbali.

Kwa upande mwingine, King'ora (2014) anaeleza kuwa taashira inaweza ikawa kitu au mfano wa kitu kinachowakilisha kitu kingine au kiumbe kisichoonekana kama vile, shetani, mungu au malaika. Hivyo, kulingana naye taashira hupatia kitu, jambo, mtu, hali, hisia au mnyama maana iliyo na uketo au hata ikapanua maana ya kawaida ama ikalipa maana mahususi neno lililoandikwa, ambayo ni tofauti na ile inayoeleweka katika hali ya kawaida na kulifanya liwe ala yenye nguvu katika kuwasilisha ujumbe. Maoni ya King'ora yalichangia ufafanuzi wa dhana ya taashira ya makala haya kuwa, taashira hutoa ujumbe zaidi ya kile kilichoandikwa au maelezo ya chombo, kama vile, meli, nahodha, bahari, dau, au mabaharia.

## MSINGI WA NADHARIA

Makala haya yaliongozwa na nguzo kuu za nadharia ya umitindo. Coombes (1953) ambaye ni mwitifaki wa nadharia hii anasema kuwa fasihi haiwezi kuchunguzwa bila kuzingatia matumizi ya lugha. Anasema kuwa mhakiki ni lazima azingatie mambo yanayofanya kazi fulani ivutie kwa kutumia lugha kwa ustadi. Ni kupitia lugha ambapo umaarufu wa mwandishi unakadiriwa. Mwandishi wa vitabu vinavyokusudiwa kusomwa na mwanafunzi wa chuo kikuu anapaswa kujiweka katika kiwango cha mwanafunzi wa chuo kikuu licha ya umahiri wake, ili aweze kuwasiliana na mwanafunzi anayemwandikia kazi hiyo. Hili hufanikishwa kupitia matumizi ya nguzo za nadharia ya umitindo ambazo ziliongoza utafiti huu. Indangasi (1988) anaelezea kwa uwazi uamilifu wa umitindo (elimu-mitindo). Anasema kwamba elimu-mitindo imesaidia kuondoa maoni yasiyo na msingi ya wahakiki kuhusu kazi ya kifasihi na hasa kuhusu lugha ya kazi hizo. Nadharia hii huwa na nguzo kadhaa lakini zilizoongoza makala haya ni tatu kuu. Nazo ni nguzo ya kiwango cha umbo, mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo pamoja na nguzo ya kiwango cha kisemantiki (Leech, 2008).

## TAASHIRA ZA WAHUSIKA KATIKA *SUDANA*

Mintarafu ya madhumuni ya makala haya, wahusika mbalimbali wa kitaashira walibainishwa na mtafiti katika tamthilia ya *Sudana*. Katika tamthilia hii, inadhihirika kuwa waandishi wametumia wahusika kitaashira ili kuwasilisha fasili tofauti tofauti za dhana moja. Ili mwandishi aweze kuwasilisha ujumbe alionuia kwa hadhira lengwa, basi hubuni na kutumia wahusika ambao kupitia kwao msomaji hujisawiri na huhukumu matokeo mbalimbali bila wasomaji wengine kuhusika. Tokeo kama lile huchangia pakubwa katika kufanikisha mawasiliano ya mwandishi kwa mpokezi bila kelele nyingi. Alamin Mazrui na Kimani Njogu walisana wahusika wafuatao kitaashira kwa minajili ya kufanikisha kazi yao.

### Sudana

Sudana ni neno linalotokana na nomino Sudan. Kiuyakinifu, Sudan ni taifa la Kiafrika. Sudana ni mmoja wa wahusika wakuu katika *Sudana*. Sudana ni mamake Sudzungu, Shume, Sizwe na wengine wengi. Wazanji waliokuwa wakimhudumia Amerigo wanamaka kutokana na hali nzuri ya Sudana. Hili laashiria uzuri wa bara la Afrika. Lakini kutokana na ulofa unaoyavaa mataifa mengi barani Afrika, mataifa yenyewe hayapendezi kamwe. Amerigo anadhibitisha kauli hii anaposema kuwa Sudana alionekana mdogo sana kama mwanamwali ilhali akina Sizwe, Sudzungu, Shume na wengine wengi walionekana wazee zaidi kuliko

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010

Sudana. Jambo hilo kama alivyokiri Amerigo lilimtatanisha kwa sabababu uhusiano ule wa mama na wanawe haukumwingia akilini. Kitaashira, yeye ni taashira ya bara la Afrika linalosheheni na kuhifadhi mataifa mengi ya Kiafrika. Pia ni taashira ya Mwafrika mzalendo. Sudana pia ni taashira ya Mwafrika mwenye huruma, upendo, utu na uzalendo. Anapoahidiwa mali, mahaba na zawadi kochokocho na Amerigo anasusia mradi asisaliti bara la Afrika na wanawe kwa jumla – Waafrika. Amerigo anapotoa amri kuwa Mzanji 5 akatwe mkono mmoja, Sudana anamtetea kwa ujasiri na ushawishi mkubwa kuashiria mapenzi ya bara la Afrika kwa mataifa yake. Hili linadhihirishwa na Sudana anapomlaani Amerigo na kusema kuwa:

> *(Kwa kelele.) Katili wee! Zimwi mla watu! Tangu maisha yetu yakumbane na yako umetudhulumu na kututendea unyama. Kumbuka hakuna baya lisilofika kikomo. Haini wee! Utakoma lini?* (uk 35).

**Amerigo**

Amerigo ni nahodha wa AMEROPE wa kabila la AMEROPE. Jina Amerigo linatokana na maneno ‘ameri’ na ‘go’. ‘Ameri’ limechotwa kutoka kwenye nomino ya pekee Amerika ambalo ni jina la taifa. Nalo neno ‘go’ ni la Kingereza cha Amerika, ambalo humaanisha ondoka au nenda. Hivyo, Amerigo ni jina linaloakisi Mwamerika anayeelekea pahali fulani. Jina AMEROPE nalo linatokana na kuunganishwa kwa sehemu za majina mawili; AMERIKA na UROPA. Uropa ni jina lingine la Ulaya. Kitaashira, Amerigo ni taashira ya viongozi wa mataifa tajiri ya Uropa na Marekani na pia ya Mbeberu dhalimu. Nahodha ni mtu anayeongoza chombo cha majini kama vile; meli na jahazi. Pia anaweza kuwa kiongozi wa kikundi cha wanamichezo kama vile, kandanda, riadha, raga na mingineyo (Mdee, Shafi, Kiango na Njogu, 2009). Nahodha kama ilivyobainika katika utafiti huu ni taashira ya kiongozi. Amerigo ni nahodha wa AMEROPE na hivyo, ni taashira ya viongozi dhalimu wa mataifa ya Amerika na Uropa.

Kwa mujibu wa Amerigo, mungu ni taashira ya Mkoloni. Hii ni kwa sababu, kulingana na Amerigo, mungu alipomuumba mwanadamu, alichukua ngoma yake kuu, akawa anaipiga kuwaita watu wa makabila mbalimbali. Kwa kufanya hivi, Amerigo alisawiri mungu kama mwenye ukabila, ubaguzi na uonevu kama Mbeberu. Amerigo alieleza kuwa kabila lililoitwa mwanzo lilikuwa lile la Wamerope ambalo lilitunukiwa akili, ilhali la mwisho lilikuwa la Wazanji ambao walifanikiwa kurithi ngoma tu kutoka kwa mungu. Hizi ni baadhi ya mbinu anazotumia Mzungu kumdhalilisha Mwafrika. Aidha, Mzungu huamini kuwa mungu ni mweupe kama yeye, na hivyo wana uhusiano wa moja kwa moja na hushikilia kauli kuwa Mwafrika alilaaniwa na kuwa mweusi. Haya hudhihirishwa kupitia filamu mbalimbali zilizochezwa na Wazungu.

Hata hivyo, ikumbukwe kwamba ngoma waliorithi Waafrika ilikuwa inatumiwa na mungu kuwasiliana na wanadamu wa makabila tofautitofauti na hivyo ni taashira ya mawasiliano yazalishayo umoja. Kadhalika, mungu aliashiriwa kama kiumbe ambaye huishiwa na kila kitu. Hii ni kwa sababu, Amerigo anasema kuwa kwa bahati mbaya au pengine nzuri, Waafrika walipofika kwa mungu alikuwa ameshamalizikiwa na kila kitu isipokuwa ngoma aliyokuwa akipiga. Hili linaashiria kuwa mungu aliachwa bila chochote na kuwa Waafrika hawakuwa wa umuhimu wowote kwake, kwani alipeana kila kitu na kuwasahau. Hakika hii ni taashira ya Mbeberu ambaye humdharau na kumdunisha Mwafrika hadi leo.

Aidha, Amerigo ni taashira ya Mbeberu; muuaji, najisi, mwenye hasira na unyama, dhalimu na mwonevu mkuu. Anaamua adhabu ya Mzanji 4 – viboko ishirini matakoni – bila kusikiliza pande zote ili kutoa uamuzi wenye haki. Anampiga Mzanji 5 bila huruma. Baada ya Mzanji 5 kueleza ukweli wa mambo. Amerigo alimuuliza Mzanji 5 kule alitoa ujeuri wa kumjibu Amerigo. Hili laashiria unyamazishaji dhidi ya Mwafrika ambao huendelezwa na Mzungu. Amerigo alishangaa kuwa Mzanji 5 alikuwa na mdomo wa kumjibu. Alimpiga makofi na mateke hadi akachoka, huku Mzanji 5 akijaribu kujikinga bila mafanikio. Hakika Amerigo alimchapa hadi akatweta kwa uchovu. Hili laashiria kuwa Waafrika ni gunia la kupigwa na Wamarekani mara tu wanapotambua kuwa Waafrika wanaweza kujinyanyua kutoka kwenye minyororo ya utumwa wa ufukara na ukoloni mamboleo. Hili linadhihirishwa kupitia maelezo ya Amerigo kwa Sudana anaeleza kuwa:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

> *Haya muondoeni mkampe adabu yake (Mabaharia waanza kutoka na Mzanji 5.). Ngonjeni! (Wanasimama.). La! Kumkata mkono si fikira nzuri; ni kumpa kisababu cha kutofanya kazi vizuri (Anafikiri kidogo). Aha! **That's it!** (Anatabasamu, akimtazama Sudana.) Mhasini! Ndiyo, mkateni dhakari yake!* (uk. 35).

Zaidi ya hayo, Amerigo ni taashira ya viongozi wauaji wa mataifa ya Magharibi. Anazaa wazo la kumuua Mzanji 5. Amerigo anapobadili wazo la kumkata mkono Mzanji 5 anatoa amri kuwa Mzanji 5 ahasiniwe – akatwe dhakari. Hakika kumkata Mzanji 5 dhakari ni kitendo cha unyama na cha kuangamiza uwezekano wowote ule wa kupata kizazi kijacho. Ukataji wa dhakari ni taashira ya mauaji ya jamii nzima barani Afrika. Ama kwa kweli, huku ni kuangamiza Waafrika wote. Hiki ni kitendo cha mauaji ya kiwango cha juu sana. Sudana anaghadhabishwa na uamuzi wake Amerigo. Baada ya Mzanji 5 kufika mbele ya Amerigo na malalamishi ya njaa, Muzungu anachochea Amerigo akasirike.

Kwa mujibu wa Mzanji 5 chakula walichokuwa wakipewa Wazanji hakikuwatosha. Muzungu anasema kuwa Wazanji wote walikuwa wajeuri na kuwaita punda ambao hawajui fadhila. Hilo lilitosha Amerigo kuamrisha Mzanji 5 akatwe mkono mmoja kwa kile alichokiita ulafi. Sudana alijaribu kumtetea Mzanji 5. Alimrejelea Amerigo kama katili. Alijaribu kumshambulia Amerigo kwa makucha lakini silisili zilimzuia na kumwangusha. Sudana alikuwa amefungiliwa kwenye kitanda. Ikizingatiwa kwamba kitandani ni mahali pa kupumzika na kustarehe, inadhihirika wazi kuwa; kitaashira dhuluma, maafa, mateso, maradhi, ulofa na mengine mengi yanayolikumba bara la Afrika; ndicho kigezo kikuu cha burudani na cha kustarehesha kwa mataifa tajiri ya Uropa na Marekani. Hii ni kwa sababu silisili zilizomfunga Sudana ni taashira ya matatizo yanayafunga mataifa fukara ya Afrika na kuyazuia kupiga hatua kisiasa, kijamii na kiuchumi. Alijaribu kukivuta kitanda bila mafanikio huku Amerigo pamoja na Wamerope wengine wakimcheka.

Mazungumzo kati ya Amerigo na Muzungu yalidhihirisha kuwa Amerigo alikuwa taashira ya mnyama kweli. Amerigo alimsononesha Sudana kwa kumrejelea kama kipenzi chake. Alijitapa kuwa alijulikana duniani kote kama nahodha mwenye huruma kabisa aliyejali maslahi ya wote bila kubagua. Kwa kweli hicho kilikuwa kinaya kwa sababu baada ya kucheka kidogo aliagiza Wamerope waliokuwa wamemshika wamuondoe wakampe adabu yake ya kukatwa mkono mmoja. Lakini ghafla akaghairi nia na kusema kuwa kumkata mkono kungempa Mzanji 5 kisababu cha kutofanya kazi na hivyo, akaagiza Mzanji 5 ahasiniwe. Amerigo alitoa ile amri akiwa na tabasamu lililomvaa usoni huku akimtizama Sudana. Yaani baada ya Amerigo kuwaza kwa muda wazo nzuri la busara na la hekima lililomjia akilini ni kumhasini Mzanji 5. Hili laashiria mawazo ya busara yanayowaziwa mataifa fukara ya Afrika na Mataifa tajiri ya Uropa na Marekani. Hakika Amerope ni katili kwa sababu, amri ya kumkata Mzanji 5 dhakari ilitekelezwa. Hili laashiria mapenzi yaliyonayo mataifa ya Uropa na Marekani juu ya mataifa fukara ya Kiafrika. Sudana alipiga kelele ambazo hakika zilikuwa za chura ambazo hazijawahi kumzuia ng'ombe kuyanywa maji. Alimkemea Amerigo na kumuita katili, zimwi mla watu na haini, maneno ambayo yaliangukia jiwe tu. Kwa mujibu wa Sudana, tangu maisha yake na ya watoto wake yalipokumbana na ya Amerigo, dhuluma na unyama ndicho chakula, kinywaji na usingizi kwake na watoto wake. Hata hivyo, Sudana hakukata tamaa kuwa siku moja wangepata afueni na kuutua mzigo wa mateso na manyanyaso.

**Muzungu**

Jina Muzungu linatokana na neno mzungu, ambalo hurejelea mtu mwenye asili ya Ulaya alimradi ni mweupe hata kama haishi au hatoki Ulaya (BAKITA, 2016). Muzungu, naibu wa Amerigo wa kabila la AMEROPE ni taashira ya viongozi wa mataifa ya Uropa pia. Kadhalika, ni taashira ya Mbeberu aliyetawala mataifa mbalimbali ya Afrika na kuyafyonza kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mabaharia wengine wa kabila la AMEROPE ni taashira za Wamarekani na Waingereza. Vilevile, Muzungu ni taashira ya Mbeberu dhalimu, mzandiki na mnyanyasaji. Anapoombwa ruhusa na Mzanji 4 anamnyima na kushikilia kauli kuwa Mzanji 4 ni mvivu ila si mgonjwa. Muzungu anampiga kofi Mzanji 5 na kumwita mwizi bila kuzingatia hali iliyompelekea Mzanji 5 kuiba viazi usiku. Baada ya Mzanji 5 kujieleza na kupigwa na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010

Amerigo, Muzungu anatia chumvi kwenye kidonda kwa kuchochea kuwa Wazanji – Waafrika – ni wajeuri, punda wasiojua fadhila.

**Sudzungu**

Sudzungu ni jina linalotokana na nomino mbili; Sudan na mzungu. Mzungu kama lilivyoelezewa hapo kabla hurejelea mtu, ilhali Sudan ni jina la taifa mojawapo la Kiafrika, ambalo huhusishwa na Waafrika weusi zaidi barani Afrika. Sudzungu, nahodha wa ZINJI wa kabila la ZANJI ni taashira ya viongozi wasaliti wa Kiafrika. ZINJI humaanisha kitu au mtu mweusi. Katika tamthilia hii ya Sudana, waandishi walirejelea watu weusi Waafrika. Kwa upande mwingine, neno ZANJI lilitumika kurejelea eneo linalosheheni watu weusi, Waafrika, yaani bara la Afrika. Kabila la ZANJI ni taashira ya Waafrika ilhali kabila la AMEROPE ni taashira ya Wamarekani na Waingereza. Mabaharia wengine wa kabila la ZANJI ni taashira ya Waafrika.

Sudzungu pia ni taashira ya viongozi wasaliti, fisadi, wanafiki na wenye ubinafsi mwingi wa mataifa ya Kiafrika. Sudzungu ni nduguye Shume na ni taashira ya viongozi wa Afrika, ambao kwa athari ya najisi kutoka kwa mataifa ya Uropa, Marekani na mengine mengi, huendelea kusaliti mataifa yao na bara la Afrika kwa jumla na kwa kila njia. Shume alidhihirisha unajisi unaoendelezwa dhidi ya mataifa ya Kiafrika na mataifa tajiri ya Uropa na Marekani. Shume alieleza Wazanji wenzake kuwa ilikuwa muhimu kumtoharisha mama yao Sudana, wamtakase na najisi iliyokuwa imempata. Bila ya kufanya hivyo, idadi ya ndugu walionajisika ingeongezeka kati yao. Mathalani, Sudzungu alikuwa mmoja wa ndugu waliokuwa wamenajisika. Shume aliwafahamisha kuwa, kutokana na athari ya najisi, ndugu wanaozaliwa huendelea kuwasaliti Waafrika kwa kila njia. Aliwahimiza wajitoe mhanga kupigania uhuru wao.

**Shume na Sizwe**

Shume, baharia wa ZINJI wa kabila la ZANJI ni taashira ya Waafrika wachache wazalendo barani Afrika. Ni mpiganiaji uhuru wa bara la Afrika kwa jumla. Shume anaashiria Waafrika wanaopigana na ukoloni mamboleo kila kuchao. Wao huzalisha mapinduzi na mabadiliko. Shume alimhimiza mamake Sudana wafanye jambo ili najisi isiweze kuwatapakaa, ikawafunika kisha ikawameza. Shume anawatia wenzake chonjo ili kupigania uhuru. Uzalendo wake unadhihirishwa na ufafanuzi wake anapoeleza kuwa: "Kwa hivyo kwanza ni lazima tumtoharishe mamaetu, tumtakase na najisi iliyompata. Bila ya hivyo, idadi ya ndugu walionajisika itaongezeka kati yetu, ndugu ambao, kwa athari ya najisi hiyo, huendelea kutusaliti kwa kila njia. Bila hivyo, kizazi chetu kitahasirika kwa miaka yote. (uk. 45).

Sizwe kwa upande mwingine ni baharia wa ZINJI wa kabila la ZANJI. Sizwe ni taashira ya wananchi Waafrika wema, watulivu, wakakamavu na washupavu. Sababu tu Sizwe alikataa kutii amri ya Amerigo, alihukumiwa kinyongo na Amerigo bila kupewa fursa ya kujitetea. Amerigo anampa Sudana uhuru wa kufanya maamuzi. Anamjuza Sudana kuwa akiitikia kufanya mapenzi naye basi maisha ya Sizwe yataokolewa na badala yake kupewa adhabu mbadala. Sizwe ambaye ni taashira ya mzalendo anapinga vikali mamake – bara la Afrika – kunajisiwa. Shume ambaye ni taashira ya Mwafrika mzalendo anaongoza katika upangaji wa mikakati ya kupigania uhuru wa bara la Afrika.

**HITIMISHO**

Alamin Mazrui na Kimani Njogu ni waandishi nguli kabisa ambao katika utunzi wa tamthilia hii ya *Sudana* walitumia mbinu ya taashira kwa kusudi la kukwepa kueleza masuala mazito paruwanja. Kimsingi, waandishi hawa walikusudia kutumia mbinu hii ili kufanikisha kuupasha ujumbe lengwa kwa hadhira lengwa. Aidha, majina mbalimbali ya wahusika hayakubuniwa kiajali ila kimakusudi. Walitumia mbinu hii kukwepa mkono wa utawala na lawama za kuuvua nguo uongozi wa kiutandawazi. Kwa kuhakiki taashira za wahusika mbalimbali huku makala yakiongozwa na nadharia ya umitindo, ilibainika kuwa masuala yaliyosawiriwa pamoja na hali tofautitofauti yalikuwepo na bado yanaendelea kujitokeza, hasa katika nchi nyingi za Afrika. Kiuyakinifu, mbinu ya taashira katika kazi za kifasihi hutumiwa kama mbinu kwepi na fiche katika kuwasilisha masuala mazito yanayoweza kuibua hisia kali, uchochezi au hata unyanyapaa katika na baina ya wanajamii.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1010

**MAREJELEO**


BAKITA (2016). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Coombes, H. (1953). *Literature and Criticism*. London: Penguin books.

Hamad, M.A. (2017).“Muundo wa Lugha Katika Mashairi ya Watungaji Wateule wa Zanzibar”. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Phd Thesis (Published).

King’ora, M. N. (2014). “Utendaji Katika Tamthilia za Sudana na Kimya Kimya Kimya”. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Indangasi, H. (1988). *Stylistics*. Nairobi. Nairobi University Press.

Leech, G. (2008). (1st ed.). *Language in Literature: Style and Foregrounding*. London:Routledge.

Mazrui, A. M. na Njogu, K. (2006). *Sudana*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Madumula, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Mbuvi, F. K. (2014). *Mwongozo wa Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora. Spotlight Publishers (EA) Limited. Nairobi.

Mdee, S., Shafi, A., Kiango, J., & Njogu, K. (2009).*Kamusi Kamili ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Nauta, D. Jr. (1972). *The Meaning of Information*. The Haque: Mouton.

Waithiru, A. K., Nabea, W. K., na Onyango, J. O. (2021). Uamilifu wa Taashira Katika Tamthilia za *Zilizala* na *Sudana Mwanga wa Lugha Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Chuo Kikuu cha Moi, Juzuu la 6 Na*. 1, 43-54. ISSN 2412-6993

Waithiru, A. K. (2022a). Symbols of the Sentient House of Usher: An Ecocritic Approach *East African Journal of Education Studies*, 5(2), 369-376. https://doi.org/10.37284/eajes.5.2.812

Waithiru, A. K. (2022b). An Evaluation of Environmental Symbolism used in Children Literature: Case Study of *Kijiji Cha Ukame* and *Mazingira Maridadi East African Journal of Education Studies*, 5(3), 1-10. https://doi.org/10.37284/eajes.5.3.846

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wilson, E. (1998). T*he Theater Experience*. New York: The McGraw-Hill Companies Inc.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.